

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 880,
Simu: (028) 2988152,
Nukushi: (028) 2988153
Barua pepe: rbckigoma@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz
Simu ya Bure : 113



TAARIFA KWA UMMA

KIGOMA – JUNI 03, 2020

MBARONI KWA KUJIFANYA AFISA WA TAKUKURU

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Kigoma inamshikilia **JAFET BRYSON EMMANUEL** mkazi wa eneo la Kilimahewa katika Manispaa ya Kigoma - Ujiji kwa makosa ya kujifanya Afisa wa TAKUKURU na Kujipatia fedha (mali) kwa njia za udanganyifu. Makosa haya ni kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007.

Uchunguzi wa TAKUKURU Mkoa wa Kigoma umebaini kwamba, Mtuhumiwa katika nyakati tofauti mwezi Mei, 2020 na katika maeneo tofauti ndani ya Manispaa ya Kigoma - Ujiji, amekuwa akijitambulisha kwamba yeye ni Afisa wa TAKUKURU kutoka ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Kigoma. Katika utambulisho wake, wapo aliowaeleza kuwa yupo TAKUKURU mkoa wa Kigoma kitengo cha sheria na wapo aliowaeleza kuwa yupo kitengo cha kushughulikia migogoro mikubwa ya ardhi.

Utambulisho wake huo uliambatana na kuomba fedha ili aweze kutekeleza majukumu yake kama Afisa wa TAKUKURU. Miongoni mwa maeneo ambayo amefika na kujitambulisha ni pamoja na Ofisi za Watendaji wa Kata za Bangwe, Businde na Kagera, Mahakama ya Mwanzo Ujiji na Ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Katika kufanikisha nia yake oву, mtuhumiwa amejipatia fedha shilingi 90,000/= kutoka kwa mwananchi (jina linahifadhiwa) ikiwa ni sehemu ya fedha shilingi 300,000/=

ambazo mtuhumiwa alimweleza mwananchi huyo kuwa ni fedha kwa ajili ya kuwezesha kutenguliwa kwa maamuzi ya Mahakama katika shauri la mgogoro wa shamba alilokuwa nalo.

Aidha mtuhumiwa aliomba fedha shilingi 500,000/= kutoka kwa mwananchi mwingine (jina linahifadhiwa) ili amsaidie kupata kazi katika ofisi za TAKUKURU. Hata hivyo mwananchi huyo hakuwa tayari kutoa fedha hizo.

Uchunguzi wa tuhuma dhidi ya mtuhumiwa unaendelea na mtuhumiwa atafikishwa mahakamani mara baada ya uchunguzi na taratibu nyingine za kisheria kukamilika.

Imetolewa na:

STEPHEN P. MAFIPA
KAMANDA WA TAKUKURU (M) KIGOMA
